# NISHATI
HABARI ZA NISHATI


# News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 51 — Juni 1 - 30, 2023



# BUNGE LAPITISHA SH. TRILIONI 3.05

## KWA AJILI YA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2023/2024





SOMA VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2023/2024 UK. WA 3


LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma




# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Mhandisi Felchesmi Mramba**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Athuman S. Mbuttuka**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma



www.nishati.go.tz
Wizara ya Nishati
@Nishati2017
wizara_ya_nishati_tanzania
Wizara ya Nishati

| | |
|---|---|
| 1. | Kupeleka umeme katika vitongoji 36,101 vilivyosalia, sawa na asilimia 56 ya vitongoji 64,760 vya Tanzania Bara. |
| 2. | Kukamilisha miradi ya uzalishaji wa umeme ikiwa ni pamoja na Miradi ya Umeme wa Maji ya Julius Nyerere (MW 2,115) na Rusumo (MW 26.67) pamoja na kutumia gesi wa Kinyerezi I Extension (MW 185). |
| 3. | Kuendelea kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme unaotokana na maji ikiwemo Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW 222), Kakono (MW 80), Malagarasi (MW 49.5); Kikonge (MW 300); umeme unaotakana na gesi wa Mtwara (MW 300), Mradi wa Mawe (MW 150) na Mradi wa Mwamba (MW 450) na miradi ya nishati jadidifu ya jotoardhi, upepo na jua. |
| 4. | Kukamilisha miradi mbalimbali ya usafirishaji wa umeme ambayo utekelezaji wake unaendelea. |
| 5. | Kuhakikisha umeme wa uhakika unaendelea kupatikana nchini kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika Mikoa ya Kagera na Katavi. |
| 6. | Kukamilisha Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu *(REA III, Round II)* ambapo umeongezwa wigo wa njia za Msongo Mdogo kutoka kilomita moja (1) hadi kilomita tatu (3) na wateja kutoka 22 hadi 66 kwa kila kijiji; pamoja na Miradi ya Ujazilizi Awamu ya IIA (Densification IIA) na Peri Urban II. |
| 7. | Kutekeleza mradi wa Ujazilizi Awamu ya IIB na IIC (*Densification IIB* na *IIC*); Peri Urban III; kusambaza umeme katika migodi midogo, maeneo ya kilimo na viwanda pamoja na kusambaza umeme katika maeneo yaliyo mbali na gridi *(off – grid projects)*. |
| 8. | Kuanza maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*, ikiwa ni pamoja na kufanya stadi za awali za utekelezaji wa mradi (*Pre-Front End Engineering Design – Pre-FEED)* na masuala ya kihandisi na kisanifu *(FEED)*. |
| 9. | Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda Hadi Tanga – Tanzania (EACOP); shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Kimkakati; usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na nchi jirani; kuimarisha matumizi ya CNG katika magari pamoja na kunadi vitalu (*licencing round*) vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini ili viendelezwe. |
| 10. | Kuendelea kutekeleza mikakati na programu mbalimbali za kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking)* nchini pamoja uanzishwaji wa vituo vidogo vya mafuta vijijini. |
| 11. | Kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia bidhaa hizo kwa kutekeleza mikakati mbalimbali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kwa manufaa ya walaji na uchumi kwa ujumla. |
| 12. | Kuendelea kuimarisha Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya TANESCO, TPDC, EWURA na PURA pamoja na Taasisi Tanzu ili yatoe huduma bora kwa mujibu wa matarajio ya wadau, kuimarisha mapato pamoja na tija na ufanisi katika uendeshaji. |
| 13. | Kuimarisha ushiriki wa wadau hususan Sekta Binafsi katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme, ikiwemo Kampuni za Africa 50, Gridworks na Larsen & Turbo na katika uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia. |
| 14. | Kuendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na rasilimali watu ya Wizara ya Taasisi zake na upatikanaji wa vitendea kazi muhimu. |

**SOMA** BAJETI YA WIZARA YA NISHATI YA MWAKA 2023/2024 KUPITIA **www.nishati.go.tz**

**SOMA** UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA BAJETI VYA MWAKA 2022/23 NA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2023/24 KUPITIA **www.nishati.go.tz**

# PICHA ZA MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WIZARA YA NISHATI ILIPOWASILISHA

## Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024,



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, akiwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bungeni, jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akijibu hoja mbalimbali za waheshimiwa Wabunge, mara baada ya Bajeti ya wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kuwasilishwa Bungeni, Jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mha.Felchesmi Mramba (wa kushoto), Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Selemani Mbuttuka, (wa pili kushoto) na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (wa tatu kushoto) wakifuatilia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati, Bungeni, jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, akiwa na Naibu Waziri wa Nishati, wakipewa hongera na waheshimiwa wabunge mbalimbali mara baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitisha, Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.*

# PICHA ZA MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WIZARA YA NISHATI ILIPOWASILISHA

## Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024,







*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Taasaisi zake wakifuatilia uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024*

# MAONESHO YA WIKI YA NISHATI JIJINI DODOMA



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (wa kwanza kushoto), akitumia kifaa maalum cha Uhalisi pepe (Virtual reality) ili kutazama maendeleo ya Mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), baada ya kutembelea maonesho ya Wizara ya Nishati kwenye viwanja vya Bunge, jijini Dodoma.*




*Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Hamis Mwinjuma, akisaini kitabu cha wageni,wakati alipotembelea banda la TANESCO la Mkoa wa Tanga katika maonesho ya Wiki ya Nishati, yaliyofanyika, jijini Dodoma kuanzia 29 Mei, 2023 hadi Juni, 01, 2023.*




*Mbunge wa Kilosa, Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi akipata maelezo katika banda la TANESCO wakati wa maonesho ya wiki ya Nishati yaliyofanyika, jijini Dodoma kuanzia 29 Mei, 2023 hadi Juni, 01, 2023.*

# MAONESHO YA WIKI YA NISHATI JIJINI DODOMA




*Mkurugenzi wa TANESCO Maharage Chande akimueleza Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge kuhusu maboresho mbalimbali ya huduma kwa wateja katika maonesho ya wiki ya Nishati yaliyofanyika, jijini Dodoma kuanzia 29 Mei, 2023 hadi Juni, 01, 2023. Kulia ni Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba*




*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akitumia kifaa maalum cha uhalisia pepe (Virtual reality) ili kutazama maendeleo ya mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP, wakati wa maonesho ya Wiki ya Nishati kuanzia 29 Mei, 2023 hadi Juni, 01, 2023.*





*Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu alipotembelea banda la TANESCO ili kupata taarifa za utekelezaji wa miradi ya umeme katika maonesho ya Wiki ya Nishati yaliyofanyika katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma kuanzia 29 Mei, 2023 hadi Juni, 01, 2023.*

# RAIS SAMIA PAMOJA NA RAIS MUSEVENI WAZINDUA MRADI WA KUFUA UMEME WA KIKAGATI – MURONGO (MW 14), MBARARA NCHINI UGANDA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan (kushoto) akivuta kamba pamoja na Rais wa Uganda Mhe. Yoweri Kaguta Museveni kuashiria uzinduzi wa Mradi wa Umeme wa Kikagati – Murongo, Mbarara nchini Uganda tarehe 25 Mei, 2023. Mradi huo wa umeme unazalisha megawati 14 ambapo kila nchi inapata megawati 7.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (wa Pili kushoto) akizungumza na Rais wa Uganda, Mhe. Yoweri Kaguta Museveni wakati walipozindua mradi wa kufua umeme wa Kikagati – Murongo (MW 14), Mbarara nchini Uganda tarehe 25 Mei, 2023.*

# RAIS SAMIA PAMOJA NA RAIS MUSEVENI WAZINDUA MRADI WA KUFUA UMEME WA KIKAGATI – MURONGO (MW 14), MBARARA NCHINI UGANDA







*Eneo la mradi wa kufua umeme wa Kikagati – Murongo (MW 14) kama linavyoonekana.*

# MAJALIWA: WATANZANIA TUMIENI NISHATI MBADALA



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), akipokea maelezo kutoka kwa Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, kuhusu vocha itakayomwezesha kuchukua mitungi ya gesi ili kuigawa kwa wananchi ikiwa ni uhamasishaji wa matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, baada ya kutembelea maonesho ya Wiki ya Nishati, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma.*

WAZIRI MKUU, Mhe. Kassim Majaliwa ametoa wito kwa Watanzania kubadilika na kutumia nishati mbadala ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Waziri Mkuu aliyasema hayo, Mei 30, 2023 baada ya kutembelea Maonesho ya Wiki ya Nishati yaliyofanyika kuanzia tarehe 29 Mei hadi tarehe 1 Juni, 2023 katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma.

Aidha, Mheshimiwa Majaliwa alisema kuwa, Wizara ya Nishati inao wajibu wa kuendelea kutoa elimu juu ya matumizi sahihi wa nishati hiyo ikiwa ni utekelaji wa maagizo ya Mhe.Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Serikali kupitia Wizara ya Nishati pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa maelekezo ya Rais, Dkt. Samia imeunda kamati ya kitaifa inayoratibu utoaji elimu na kuonesha fursa za wajasiriamali ambao watahitaji kuingia kwenye sekta hii ya matumizi ya nishati mbadala."

"Anzeni na taasisi za elimu, majeshi, kambi za wakimbizi na kila mahali ambapo panakaliwa na watu zaidi ya mia moja, nataka sasa maeneo hayo yawe anzilishi na tuachane na kukata miti. Tunataka watanzania waanze kutumia nishati mbadala, huu ndio muelekeo wa Taifa letu."

Pia, alitoa rai kwa wajasiriamali kuendelea kubuni na kutengeneza nishati mbadala kwa kutumia rasilimali mbalimbali zilizopo nchini ikiwemo vumbi la makaa ya mawe na pumba za mahindi.

Katika hatua nyingine, Mheshimiwa Majaliwa aliupongeza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kuendelea kuhakikisha wanaratibu mpango kupeleka umeme vijijini.

"Wale mliopewa jukumu la kusimamia hili, jiridhisheni na kuhakikisha kila kijiji kinapata umeme, na muwasimamie wakandarasi ili wafanye kazi hiyo kikamilifu."

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati, Januari Makamba alisema wizara hiyo imejipanga kutumia makundi mbalimbali katika kuhamasisha Watanzania juu ya matumizi ya nishati mbadala. "Pamoja na hili Wizara ifikapo Julai 2023 itazindua dira ya Nishati Safi ya kupikia"



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (wa kwanza kulia) na Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (wa pili kulia), wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kuja na Kushoka Tools Manufactures Group inayotengeneza mkaa mbadala, Bw. Leonard Kushoka (kushoto), wakati alipotembelea mabanda ya maonesho ya Wiki ya Nishati kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma, Mei 30, 2023.*




*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake (hawapo Pichani), mara baada ya kutembelea maonesho ya Wiki ya Nishati kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma, Mei 30, 2023. Kulia ni Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba.*

# NISHATI SAFI YA KUPIKIA NI KIPAUMBELE CHA NCHI - WAZIRI MKUU

**Teresia Mhagama na Zuena Msuya**

Waziri Mkuu, Mhe.Kassim Majaliwa amesema kuwa, suala la upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ni moja ya vipaumbele vya nchi na kwamba Serikali inahakikisha kuwa uandaaji wa Dira na Mpango Mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia unafanyika kwa kasi na kwa umakini ili kuanza kutekeleza azma hiyo.

Alisema hayo tarehe 19 Mei, 2023 jijini Dodoma wakati akiongoza Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba ambae ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri ya Kikundi Kazi hicho. Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo pia walihudhuria.

Kikao hicho ambacho ni cha ngazi ya Kamati ya Mawaziri ya Kikundi Kazi cha Nishati Safi ya Kupikia kilikuwa mahsusi kwa ajili ya kujadili rasimu ya Dira ya Taifa ya Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia 2033 na Mpango Mkakati wa utekelezaji wake pamoja na rasimu ya mapendekezo ya uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia, taarifa ya uchambuzi wa miongozo mbalimbali inayohusu nishati safi ya kupikia pamoja na maboresho yaliyofanyika baada ya kikao cha Waziri Mkuu kilichofanyika tarehe 23 Machi, 2023.

"Serikali imeamua kwenda nalo kasi suala hili la nishati safi ya kupikia ili kuepusha uharibifu wa mazingira kwani nishati ambayo si salama kama kuni na mkaa inatumika kwa kiasi kikubwa kwa kupikia hivyo tutakapoanza kutekeleza Dira hii, kwa kiasi kikubwa tutapunguza uharibifu wa mazingira pamoja na kulinda afya za wananchi." alisema Waziri Mkuu

Waziri Mkuu, aliipongeza Kamati ya Uongozi ya Makatibu Wakuu inayoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutoa mwongozo na maelekezo yaliyosaidia kuboresha nyaraka hizo muhimu. Aidha, aliwapongeza Kamati ya Wataalamu pamoja na Sekretarieti ya Kikundi Kazi kwa maandalizi ya nyaraka hizo.

Aidha, aliiagiza Kamati ya Wataalamu ya Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ijumuishe maoni yote yaliyotolewa yakiwemo ya Wadau wa Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo ili kuboresha Dira na Mpango Mkakati na ziwasilishwe ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 26 Mei 2023.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba alisema kuwa, kikao hicho kilichoshirikisha wadau kutoka Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo kimepokea maoni yaliyotolewa kwenye kikao hicho ambayo yatasaidia kuboresha rasimu hizo za Dira ya Taifa ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Dira hiyo, Muundo wa Mfuko wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia na Taarifa ya Uchambuzi wa Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali inayohusika na nishati ya kupikia ili kuweka uwiano.

Alisema kuwa, suala la utekelezaji wa Nishati Safi ya Kupikia limezingatia miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs-2030) ambapo lengo namba 7 linazungumzia masuala ya upatikanaji wa nishati safi na bei nafuu. Makamba alisisitiza kuwa Dira hii inakataza matumizi ya mkaa wa asili ambao una athari kwa afya na mazingira, hivyo uwekezaji katika mkaa mbadala wenye viwango vinavyotakiwa uendelee.



*Waziri Mkuu, Mhe.Kassim Majaliwa (katikati) akiongoza Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba, Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi Mei 19, 2023, jijini Dodoma. Kulia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama na kushoto ni Waziri wa Nishati, January Makamba.*



*Waziri Mkuu, Mhe.Kassim Majaliwa (pili kushoto) akizungumza wakati wa Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba, Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi Mei 19, 2023, jijini Dodoma.*



*Baadhi ya Mawaziri waliohudhuria Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba, Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi Mei 19, 2023, jijini Dodoma. Kulia ni Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe.Angellah Kairuki na Waziri wa Madini, Mhe.Dkt.Doto Biteko( katikati).*




*Waziri Mkuu, Mhe.Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Meneja Mauzo wa Kampuni ya Consumer's Choice Limited, Isack Danford (kulia) kuhusu nishati safi ya kupikia baada ya kuongoza Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba, Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi Mei 19, 2023, jijini Dodoma. Kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Mhe.Jenista Mhagama na wa tatu kushoto ni Waziri wa Nishati, January Makamba.*



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba akizungumza wakati wa Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba, Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi Mei 19, 2023, jijini Dodoma*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akizungumza wakati wa Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba, Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi Mei 19, 2023, jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Kheri Mahimbali ( kushoto) na wadau wengine wa Nishati Safi ya Kupikia wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati wa Kikao cha Tatu cha Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya kupikia ambacho kilishirikisha Mawaziri wanaosimamia sekta zinazohusika na mradi huo wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba, Makatibu Wakuu wa Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau kutoka Sekta Binafsi Mei 19, 2023, jijini Dodoma*

# MKATABA WA KWANZA WA UZALISHAJI UMEME JUA (MW 50) WASAINIWA

**Teresia Mhagama na Godfrey Mwemezi**

Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imesaini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

Mkataba huo umesainiwa tarehe 29 Mei, 2023 jijini Dodoma na kushuhudiwa na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba ambaye alikuwa mgeni rasmi.

Kwa ujumla mradi huo wa umeme wa Jua ni wa megawati 150 ambapo awamu kwanza itajengwa mitambo itakayozalisha megawati 50 na awamu ya pili itajengwa mitambo ya megawati 100 kwa jumla ya shilingi bilioni 275.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Nishati amesema kuwa "kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi tunaingiza umeme wa Jua katika gridi ya Taifa, nimpomgeze Rais wetu kwa kwa muongozo na uongozi ambao umepelekea nchi kuaminiwa na washirika wa maendeleo ikiwemo Shirika la Maendeleo la Ufaransa ambalo limetoa mkopo ambao utatekeleza mradi huu."

Ameeleza kuwa, utekelezaji wa mradi huo wa Jua ni jitihada za Serikali za kuhakikisha inatengeneza mchanganyiko wa umeme wenye afya katika gridi ya Taifa ambao utatokana na vyanzo mbalimbali kama vile maji, gesi, upepo na Jua ili hata pale chanzo moja kinapotetereka, vyanzo vingine vitaendelea kuzalisha umeme.

Waziri Makamba amesema kuwa, ili kuongeza zaidi uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati jadidifu, Serikali inakuja na Sera mpya ya Nishati Jadidifu (iko kwenye maandalizi) ambayo itasaidia nchi kuongeza uwekezaji kwenye eneo hilo kwani fedha nyingi duniani, masoko ya mitaji na teknolojia mpya zinajielekeza kwenye nishati jadidifu.

Ameongeza kuwa, kwa sasa kazi inayofanyika pia ni kuainisha maeneo yaliyo na rasilimali ya nishati jadidifu na kipaumbele kitakuwa kwa wazawa kuwekeza kwenye miradi kama ya Upepo na Jua na Serikali itawaunga mkono na kwamba Serikali itakuja na muongozo wa utekelezaji wa suala hilo.

Ameongeza kuwa, kwa maeneo yaliyo nje ya gridi kama vile visiwa, bado Serikali itaendelea kuwezesha jitihada za kupelewa umeme kwa kutumia miradi ya nishati jadidifu kama vile Jua na Upepo.

Akitoa taarifa ya mradi huo wa umeme Jua, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande amesema awamu ya kwanza itajumuisha ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa teknolojia ya solar photovoltaic kwa ukubwa wa megawati 50 na ujenzi wa kituo kipya cha kuongeza umeme msongo wa kilovolti 33/220 ikiwa ni pamoja na kuunganisha kituo hicho kwenye gridi ya Taifa kwa msongo wa kV 220 kwenye laini ya kutoka Singida hadi Shinyanga.

Amesema kuwa mkandarasi mjenzi wa mradi huo wa Awamu ya Kwanza ni kampuni ya Sinohydro corporation ya nchini China na Mkandarasi mshauri ni kampuni ya




*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (katikati) akishuhudia utiaji saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga. Wanaotia saini ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande (kulia) na Mwakilishi Mkuu wa kampuni ya Sinohydro nchini Tanzania, Shi Yong. Kushoto kwa Waziri ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme.*




*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (katikati) akishuhudia watendaji kutoka TANESCO (kulia) na kampuni ya Sinohydro ya China (kushoto) wakikabidhiana mikataba ya utekelezaji wa mradi wa umeme Jua utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga. Kushoto kwa Waziri ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme.*

# MKATABA WA KWANZA WA UZALISHAJI UMEME JUA (MW 50) WASAINIWA

JV Artelia ya Ufaransa na Energiovida ya Tanzania na gharama za mradi ni shilingi Bilioni 109.

Amesema kuwa mradi huo wa awamu ya kwanza utekelezaji wake hautazidi miezi 12.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme amemshukuru Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan, Wizara ya Nishati na TANESCO kwa mradi huo na ameahidi kuwa watawapa ushirikiano wakandarasi wa mradi ili watekeleza mradi huo kwa wakati na pia kuutunza ili uweze kunufaisha wananchi wa Shinyanga na Tanzania kwa ujumla.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe.Judith Kapinga amemshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya Nishati nchini

Amepongeza Wizara na TANESCO, kwa kubuni miradi mbalimbali ambayo itapelekea nchi kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika.

Kwa upande wake, Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo amepongeza kwa mradi huo ambao amesema kuwa utakuwa na manufaa makubwa kwani pamoja na kupata umeme katika maeneo mbalimbali kama migodi, mradi huo utafaidisha wananchi wanaozunguka mradi kwa kupata huduma za kijamii kama shule na maji.

Viongozi wengine waliohudhuria hafla hiyo ni Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Wabunge wa Mkoa wa Shinyanga, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga.



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*




*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*



*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rose Senyamule akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*



*Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*



*Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Judith Kapinga akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*



*Mbunge wa Kishapu, Mhe. Boniphace Butondo akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa kwanza wa uzalishaji wa umeme Jua wa kiasi cha megawati 50 utakaotekelezwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.*

# MAKAMBA AKUTANA NA BALOZI WA INDOSESIA NA VIONGOZI WA KAMPUNI YA PERTAMINA

**Na Zuena Msuya DSM,**

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amefanya mazungumzo na Balozi wa Indonesia nchini Tanzania,Tri Yogo Jotmiko na Viongozi Waandamizi wa Kampuni ya Kimataifa ya Uwekezaji ya Pertamina ya nchini Indonesia akiwemo Rais wa Kampuni hiyo John Anis.

Mazungumzo hayo yalifanyika Mei 16, 2023 jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuzungumzia suala la kampuni ya Maurel & Prom ambayo inamilikiwa na Kampuni ya Pertamina kwa asilimia 100 kununua hisa za Kampuni ya Wentworth Resources ambaye ni mbia katika Kitalu cha Mnazi Bay mkoani Mtwara.

Makamba alimweleza Balozi wa Indonesia na viongozi hao kuwa, Tanzania imeweka mazingira rafiki katika suala zima la uwekezaji hivyo kuhusu maombi yao, alielekeza Taasisi zinazohusika na suala hilo ikiwemo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kukutana kwa pamoja ili kutazama suala hilo na kuishauri Serikali kama Sheria inavyoelekeza.

Viongozi wengine walioshiriki katika Kikao hicho ni Balozi wa Tanzania nchini Indonesia, Macocha Tembele, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mussa Makame na Viongozi wengine wandamizi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Kampuni ya Maurel & Prom imeonesha nia ya kununua hisa za Wentworth Resources ambaye ni mbia mwenza kwenye kitalu cha Mnazi Bay. Ununuzi huo utapelekea mabadiliko katika uendeshaji wa kitalu hicho (change of control) na kuongeza hisa za Maurel & Prom kutoka 48% za sasa hadi 80%, mbia mwingine katika kitalu hiki ni TPDC mwenye asilimia 20 ya hisa.



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akiongoza kikao baina ya Balozi wa Indonesia nchini Tanzania, Tri Yogo Jotmiko (wa pili kushoto) na Viongozi Waandamizi wa Kampuni ya Kimataifa ya Uwekezaji ya Pertamina ya nchini Indonesia, akiwemo Rais wa Kampuni hiyo, John Anis (wa tatu kushoto) kilichofanyika Mei 16, 2023 jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akimsikiliza Balozi wa Indonesia nchini Tanzania, Tri Yogo Jotmiko (katikati) na Rais wa Kampuni ya Kimataifa ya Uwekezaji ya Pertamina ya nchini Indonesia, John Anis (kushoto) wakati wa kikao kuhusu nia ya kampuni ya Maurel & Prom kununua hisa za mbia mwenza Wentworth resources katika Kitalu cha kuzalisha Gesi Asilia cha Mnazi Bay mkoani Mtwara kilichofanyika Mei 16, 2023 jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (tatu kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Indonesia nchini Tanzania, Tri Yogo Jotmiko (wa pili kulia), Rais wa Kampuni ya Kimataifa ya Uwekezaji katika sekta ya Mafuta na Gesi ya Pertamina ya nchini Indonesia, John Anis (kulia), Balozi wa Tanzania nchini Indonesia, Macocha Tembele,( tatu kushoto) Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mussa Makame( wa pili kushoto) baada ya kumaliza kikao hicho kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizoko jijini Dar es Salaam.*

# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA PETROLI WA AFRIKA MASHARIKI KWA MAFANIKIO




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba akizungumza katika Maonesho na Mkutano wa Kumi (10) wa Petroli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'23) uliofanyika nchini Uganda.*

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa Nishati wameshiriki Maonesho na Mkutano wa Kumi (10) wa Petroli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'23) ambapo Tanzania ilifanikiwa kutangaza fursa za uwekezaji na ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

Mkutano huo uliofanyika Kampala, nchini Uganda kuanzia tarehe 9 – 11 Mei, 2023, ulishirikisha nchi saba za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Makatibu Wakuu wa nchi husika walieleza maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi na kutangaza fursa za uwekezaji katika nchi zao kwa wadau mbalimbali walioshiriki Mkutano huo zikiwemo Kampuni za Kimataifa za mafuta na gesi, mabenki, kampuni za kodi, bima na watoa huduma mbalimbali.

Kwa upande wa Tanzania Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba alieleza kuhusu fursa hizo zinazopatikana nchi Tanzania na kukaribisha wawekezaji nchi kuja kuendeleza rasimali ya mafuta na gesi.

Ujumbe wa Tanzania ulijumuisha viongozi mbalimbali wakiwemo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. Dunstan Kitandula; Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya; Mwenyekiti wa Bodi za PURA, Halfani R. Halfani pamoja na wakuu wa Taasisi na wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango, Taasisi za Serikali na wawekezaji kutoka sekta binafsi.

Mkutano huo pia ulijadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya mafuta na gesi hususan mjadala unaoendelea wa kuhamia katika nishati safi (Energy Transition). Hivyo, Mkutano uliazimia matumizi ya nishati safi na uendelezaji bora wa rasilimali za mafuta na gesi kwa kutumia teknolojia za kisasa kwa lengo la kuhakikisha uwepo na upatikanaji wa nishati ya kutosha na endelevu kwa kuzingatia usalama wa mazingira.

Kwa mujibu wa makubaliano ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mikutano kama hii hufanyika kila baada ya miaka miwili kwa kupokezana baina ya nchi Wanachama. Hivyo, Tanzania ilitumia Mkutano huo kuongeza uzoefu katika kujiandaa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kumi na Moja (11) wa Petroli wa Afrika Mashariki (EAPCE'25) unaotarajiwa kufanyika nchini Tanzania.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe.Dunstan Kitandula akizungumza katika Maonesho na Mkutano wa Kumi (10) wa Petroli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'23) uliofanyika nchini Uganda.*




*Wataalam kutoka Wizara ya Nishati wakiwa katika Maonesho na Mkutano wa Kumi (10) wa Petroli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'23) uliofanyika nchini Uganda.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa Tano kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watendaji kutoka Wizara ya Nishati wakati wa Mkutano wa Kumi (10) wa Petroli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'23) uliofanyika nchini Uganda. Wa Sita kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandula na wa Nne kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kushoto) na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe.Dunstan Kitandula wakiingia katika Mkutano wa Kumi (10) wa Petroli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'23) uliofanyika nchini Uganda.*

# MAKAMBA AFANYA MAZUNGUMZO NA KAMPUNI ZITAKAZOTEKELEZA MRADI WA LNG

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amekutana na Viongozi wa Kampuni zitakazotekeleza Mradi wa kuchakata na kusindika Gesi ya Asilia (LNG).

Makamba amekutana na viongozi hao ambao ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Medco Energi, Roberto Lorato, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Pavilion Energy ltd, Alan Heng pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Shell nchini Tanzania, Jared Kuel kwa lengo la kujadili maendeleo ya maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa LNG.


Mkutano huo ulifanyika Aprili 9,2023 jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mussa Makame na viongozi wengine waandamizi kutoka Wizara ya Nishati.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wenzake, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Medco Energi, Roberto Lorato amesema kampuni hizo ziko tayari kuanza utekelezaji wa mradi huo mara baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Kwa upande wake, Waziri Makamba amezihakikishia kampuni hizo kuwa Serikali iko tayari kuutekeleza mradi huo Mkubwa na wa kimkakati kwa manufaa makubwa nchini.

Alifafanua kuwa, mradi huo utakaogharimu zaidi ya shilingi Trilioni 70 za kitanzania ni muhimu kwa taifa katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo zaidi.

Vilevile aliwahakikishia wawekezaji kuwa Serikali imeanza maandalizi ya utekelezaji wa Mradi kwa kuanzisha Ofisi Maalum (LNG Project Office)ili kurahishisha uratibu wa masuala yote ya Mradi.



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba ( katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Medco Duniani, Roberto Lorato (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Pavilion Energy ltd, Alan Heng wakati wa kikao cha kujadili maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusindika Gesi Asilia (LNG) kilichofanyika mkoani Dodoma , Aprili 9,2023.*



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (kushoto) akiongoza kikao kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusindika Gesi Asilia( LNG), kilichowashirikisha Wawekezaji watakaotekeleza Mradi huo waliopo upande wa kulia ambao Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Medco Energi, Roberto Lorato, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Pavilion Energy ltd, Alan Heng, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Shell nchini Tanzania, Jared Kuel, upande wa kushoto kwa Waziri ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Athuman Mbuttuka, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania(TPDC) Mussa Makame na viongozi wengine waandamizi kutoka Wizara ya Nishati, kilichofanyika mkoani Dodoma , Aprili 9,2023.*



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wawekezaji watakaotekeleza Mradi wa kusindika Gesi Asilia (LNG) ambao ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Medco Energi, Roberto Lorato,(kulia kwa Waziri), Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Pavilion Energy ltd, Alan Heng, (kushoto kwa Waziri Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Shell nchini Tanzania, Jared Kuel, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Athuman Mbuttuka, (wa tatu kulia) , Viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania(TPDC), kilichofanyika mkoani Dodoma , Aprili 9,2023.*

# TANZANIA NA JICA KUSHIRIKIANA KATIKA KUJENGA UWEZO WA MATUMIZI BORA YA GESI ASILIA

Wizara ya Nishati pamoja Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA) wamesaini makubaliano ya kutekeleza mradi wa kujengea uwezo Wataalam wa Wizara na Taasisi zake katika eneo la kuendeleza matumizi bora ya Gesi Asilia ili kuiwezesha Tanzania kuendelea kunufaika kiuchumi na rasilimali hiyo.

Makubaliano hayo yalisainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba na Mwakilishi Mkuu wa JICA Tanzania, ARA Hitoshi tarehe 16 Mei, 2023 jijini Dar es Salaam.

Makubaliano hayo yatapelekea wataalam wa Tanzania kuongeza ufanisi katika kufanya mipango na kutekeleza miradi ya matumizi ya Gesi Asilia kwa kuzingatia pia suala la utunzaji wa mazingira.




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kushoto) na Mwakilishi Mkuu wa JICA Tanzania, ARA Hitoshi wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kusaini makubaliano ya kutekeleza mradi wa kujengea uwezo Wataalam wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake katika eneo la kuendeleza matumizi bora ya Gesi Asilia.*

# KAMATI YA USIMAMIZI JNHPP YAKAGUA MRADI



*Mwenyekiti ya Kamati ya Usimamizi wa Mradi wa umeme wa Julius Nyerere ambaye pia ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. Jim Yonaz (kushoto) akiongoza kikao cha kamati hiyo wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, Mei 14, 2023 mkoani Pwani.*

**Na Zuena Msuya**
**Pwani,**

Kamati ya Usimamizi wa Mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) imekagua mradi huo na kutoa wito kwa watanzania kuendelea kuunga mkono utekelezaji wa mradi kwakuwa una faida kubwa kwa nchi na watanzania.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti ya Kamati ya Usimamizi wa mradi huo ambaye pia ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. Jim Yonaz wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo, Mei 14, 2023 mkoani Pwani.

Ziara hiyo imehusisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Makatibu Wakuu kutoka Wizara mbalimbali zinazohusika moja kwa moja katika utekelezaji wa mradi huo, Kamishna wa umeme na Nishati Mbadala kutoka Wizara ya Nishati(CERE), Mhandisi Innocent Luoga pamoja na viongozi waandamizi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Dkt. Yonaz alisema kuwa mara baada ya mradi huo kukamilika na kuanza kuzalisha umeme, mafanikio mengine makubwa yatapatikana katika sekta ya Uvuvi, Kilimo na Utalii na hivyo kukuza uchumi wa nchi na watanzania kwa jumla.

Aidha, ameipongeza Wizara ya Nishati na TANESCO kwa kazi kubwa ya usimamizi na utekelezaji wa mradi huo kwa hatua iliyofikiwa ambayo inatoa picha halisi kwa jamii, kuwa muda si mrefu umeme utaanza kuzalishwa.

Kwa upande wake Katibu wa Kamati hiyo ambaye pia ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alieleza kuwa hatua ya ujenzi wa mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 86.8 na kazi ya ujenzi inaendelea na matarajio ni kuanza kuzalisha umeme Juni 2024.

"Maendeleo ya mradi ni mazuri sana ikilinganishwa na kipindi kile ambacho Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuja kuzindua rasmi zoezi la ujazaji maji katika bwawa hilo ambao eneo tulilokuwa tumekaa wakati ule kwa sasa limekuwa na maji yenye kina cha mita 30, kwa hiyo haiwezekani kufika pale tena, hiyo ni ishara inayoonesha maendeleo makubwa", alisema Mhandisi Mramba.

alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha na maelekezo ambayo yamewezesha mradi huo kufikia hatua hiyo, wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha wanaohakikisha malipo yanafanyika kwa wakati na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kusafirisha mitambo ya mradi huo.

Kamati hiyo ilitembelea eneo la Kingo za Bwawa husika, Tuta kuu la Bwawa, nyumba ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme na njia ya kupeleka maji ya kuzungusha mitambo ya kuzalisha umeme, pamoja na eneo la ufungaji wa mitambo.



*Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Kufua umeme wa Julius Nyerere, Mei 14, 2023 mkoani Pwani.Wa nane kulia ni Mwenyekiti ya Kamati hiyo ambaye pia ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. Jim Yonaz na kushoto kwakwe ni Katibu wa Kamati hiyo ambaye pia ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.*



*Katibu wa Kamati ya Usimamizi wa Mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambaye pia ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba,(wa tatu kushoto) akiwaeleza jambo, Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huo, Mei 14, 2023 mkoani Pwani.*



*Vijana walioonekana wakiendelea na kazi katika nyumba ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme wa Julius Nyerere, wakati wa ziara ya Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa mradi wa Julius Nyerere ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi husika, Mei 14, 2023 mkoani Pwani.*



*Muonekano wa ujazo wa maji katika eneo la njia ya kupeleka maji ya kuzungusha mitambo ya kuzalisha umeme wa Julius Nyerere, ilivyoonekana wakati wa ziara ya Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa mradi huo ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi husika, Mei 14, 2023 mkoani Pwani.*

# KATIBU MKUU NISHATI AFANYA MAZUNGUMZO NA MWAKILISHI MKAZI WA IMF

**Teresia Mhagama na Godfrey Mwemezi**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amekutana na kufanya mazungumzo na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nchini Tanzania, Jens Reinke na watendaji wengine wa Shirika hilo ambapo kikao hicho kililenga kujadili masuala mbalimbali ikiwemo mwenendo wa uchumi, utekelezaji wa bajeti, mipango ya maendeleo ya nchi na program ya ufadhili wa miradi (ECF).



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa kwanza,kushoto), na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nchini Tanzania, Jens Reinke (wa Pili kutoka kulia) wakiwa katika kikao kilichofanyika jijini Dodoma tarehe 2 Juni, 2023. Wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, TPDC na IMF*

Kikao hicho kilifanyika jijini Dodoma tarehe 2 Juni, 2023 na kuhudhuriwa na Kamishna wa umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga, Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mussa Makame na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati na TPDC.

Katika kikao hicho, Mhandisi Mramba aliwaeleza watendaji hao kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali itakayopelekea nchi kuwa na umeme wa kutosha na uhakika ukiwemo mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2,115, unaotarajiwa kukamilika mwezi Juni 2024.



*Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent luoga akiwa katika kikao cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (hayupo pichani) na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nchini Tanzania, Jens Reinke (hayupo pichani kulia).*

Katibu Mkuu pia aliwaeleza watendaji hao kuhusu Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG) ambao ameeleza kuwa, majadiliano yake ya Mkataba wa Nchi Hodhi (HGA) na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanywaji Mapato (PSA) kati ya Timu ya Majadiliano ya Serikali na Wawekezaji katika Vitalu husika yamekamilika.

Vilevile, aliwaeleza watendaji wa IMF kuhusu hatua zinazoendelea kufanyika katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) ambao alisema kuwa kwa ujumla unaendelea vizuri.

Aidha, aliwaeleza watendaji hao kuhusu hatua mbalimbali ambazo Serikali imezifanya hadi sasa za kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili ifikapo mwaka 2033, asilimia 80 ya wanachi wawe wanatumia nishati hiyo.

Katibu Mkuu pia alitanabaisha kuhusu vyanzo vya nishati jadidifu vilivyopo nchini ikiwemo Jua na Upepo ambavyo alisema kuwa, wawekezaji mbalimbali wanaweza kuvitumia kuzalisha umeme.

Katibu Mkuu aliishukuru IMF kwa kutoa fedha shilingi Bilioni 200 kupitia mpango wa ECF kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa pamoja na kupeleka umeme katika vitongoji vya mikoa ya Songwe na Kigoma.

Kwa upande wake, Mwakilishi Mkazi wa IMF nchini Tanzania, Jens Reinke alimshukuru Katibu Mkuu kwa kupata taarifa hizo muhimu ambazo wao kama wadau zinawasaidia katika kufahamu mwelekeo wa Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.



*Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja (wa kwanza kushoto) pamoja na watendaji kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) wakiwa katika kikao cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (hayupo pichani) na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nchini Tanzania, Jens Reinke (hayupo pichani kulia).*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa tatu kushoto) na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nchini Tanzania, Jens Reinke (wa nne kutoka kulia) wakiwa katika picha ya pamoja na watendaji wa Wizara ya Nishati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na IMF baada ya kikao kilichofanyika jijini Dodoma tarehe 2 Juni, 2023.*

# MIRADI YA NISHATI KUIMARISHIWA ULINZI

**Na.Timotheo Mathayo, Dodoma.**

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa wamekutana kwa ajili ya kupanga mikakati ya kuimarisha ulinzi kwenye miradi ya kimkakati inayosimamiwa na Wizara ya Nishati.

Kikao hicho kilifanyika 04 Mei, 2023 Jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Faraji Mnyepe, Maafisa kutoka Wizara ya Nishati,Jeshi la Wananchi (JWTZ) pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) .

Waziri Makamba alisema kuwa Wizara ya Nishati inatekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati ukiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere unaotegemea kuzalisha jumla ya Megawati 2,115.

Pamoja na Mradi wa ujenzi wa bomba la Mafuta ghafi (EACOP), maandalizi ya Mradi wa kuchakata na kusindika gesi Asilia wenye thamani ya zaidi ya Trilioni 70 pamoja na baadhi ya Miradi ya kusambaza Umeme Vijijini inayotekelezwa na Kampuni ya SUMA JKT Electric Campany limited.

Aidha, Waziri Makamba aliipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa ushirikiano wanaotoa katika kutekeleza na kuimarisha ulinzi kwenye miradi ya kimkakati.

Kwa upande wake, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe.Innocent Bashungwa ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano katika suala la kuimarisha ulinzi kwenye miradi yote ya kimkakati inayosimamiwa na Wizara ya Nishati.

“Sisi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa tunawaahidi kuwapa ushirikiano mkubwa katika kuendelea kulinda na kutekeleza miradi ya kimkakati nchini” alisema Bashungwa.



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (mbele, Kulia), akifafanua jambo mbele ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa (kushoto) pamoja na watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati , Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).*

# WABUNGE WAPATA ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Na.Timotheo Mathayo, Dodoma**

Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamepata elimu kwa kina ya nishati safi ya kupikia ambayo imejumuisha pia Rasimu ya Dira ya Taifa ya Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia na Mpango Mkakati wa utekelezaji wake lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2033.

Wabunge hao walipata elimu hiyo tarehe 27 Mei, 2023 jijini Dodoma katika Semina iliyoandaliwa na Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na kuongozwa na Waziri wa Nishati,

Waziri wa Nishati, January Makamba alisema kuwa takriban asilimia 85 ya watanzania wanatumia nishati ya Tungamotaka ambayo inajumuisha kuni, mikaa, magogo, mabaki ya mazao na vinyesi vya wanyama ambapo asilimia 72 ya nishati yote nchini inatumika majumbani na si viwandani au katika usafirishaji.

"Asilimia kubwa ya nishati inayotumiwa na watanzania ni tungamotaka na inatumika majumbani kwa kupikia kwa hiyo kuzungumzia tu mitambo ya kuzalisha na kusafirisha umeme, gesi au mafuta haitoshi kwani watanzania wengi wanatumia nishati ya kupikia ambayo ni ya tungamotaka hivyo ili kutendea haki kazi tulizopewa tumeona lazima tuingilie kati kwenye nishati safi ya kupikia na hilo ndio chimbuko la kulipa nguvu suala hili."alisema Makamba

Waziri wa Nishati alitaja athari mbalimbali zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo salama ikiwemo ya vifo takriban 33,000 kwa mwaka vinavyotokana na magonjwa ya mfumo wa kupumua unaotokana na moshi wa nishati isiyosafi kwa kupika, athari za mazingira kutokana na ukataji wa kuni na uchomaji wa mkaa pamoja na athari za kijamii.

" Suala la nishati safi ya kupikia ni utekelezaji wa Sera ya Nishati ya mwaka 2015 ambayo inasema kwamba Serikali itachukua hatua mahsusi za kuwasaidia watanzania ili wahame kutoka kwenye nishati isiyo safi na salama kwenda kwenye nishati ya kisasa na safi, hivyo hapa tunatekeleza Sera ya Nishati ."Alisema Makamba

Amesisitiza kuwa, utekelezaji wa Nishati Safi ya Kupikia unalenga kuleta ustawi wa kinamama na watanzania na si nadharia na ndio maana Serikali imelibeba kwa nguvu kubwa suala hili ambapo aliongeza kuwa asilimia tano tu ya watanzania kwa sasa ndio wanatumia nishati safi ya kupikia.

Akizungumzia kuhusu matumizi ya gesi ya mitungi, alisema kuwa ni salama.

Waziri Makamba alitoa wito kwa wabunge kuhamasisha wananchi kutumia nishati hiyo na kuwapatia Wabunge vocha za mitungi ya gesi 100 kila mmoja lengo likiwa ni kusaidia kuhamasisha kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuwa mitungi ya gesi ya kupikia ni salama wananchi wasihofu kuitumia.

Katika hatua nyingine, Waziri Makamba aliwakaribisha Wabunge hao katika Maonesho ya Wiki ya Nishati yatakayoanza tarehe 29 Mei hadi tarehe 01 Juni, 2023 katika Viwanja vya Bunge jijini Dodoma na kueleza kuwa, Maonesho hayo pia yatatumika kutoa taarifa ya miradi mbalimbali ya nishati na kutoa utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazohusu Sekta kwani viongozi Wakuu wa Wizara pamoja na Taasisi watakuwepo katika Maonesho hayo.

Katika Semina hiyo pia wabunge walipata uelewa zaidi kuhusu hali ya upatikanaji umeme, utekelezaji wa miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme pamoja na usambazaji wa nishati safi ya kupikia katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa upande wao, Wabunge hao wakiongozwa na Mhe.Dunstan Kitandula ambaye alimwakilisha Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wamepongeza kwa semina hiyo ambayo imewapa uelewa wa utekelezaji wa miradi mbalimbali na walitoa maoni mbalimbali yatakayofanyiwa kazi na Wizara.

Waziri Makamba aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na viongozi wengine wa Wizara ya Nishati, REA na TANESCO.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe.Dunstan Kitandula akizungumza wakati wa semina ya kuwajengea uelewa wabunge katika sekta ya Umeme na Nishati Safi ya Kupikia*




*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza jambo wakati wa semina ya kuwajengea uelewa wabunge katika sekta ya Umeme na Nishati Safi ya Kupikia, iliyofanyika Jijini Dodoma, Mei 27, 2023.*




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akifuatilia uwasilishaji wa hoja mbalimbali za Wabunge wakati wa semina ya kuwajengea uelewa katika sekta ya Umeme na Nishati Safi ya Kupikia, iliyofanyika Jijini Dodoma, Mei 27, 2023.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ( wa pili kulia), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe.Dunstan Kitandula (wa kwanza kulia), Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Selemani Mbuttuka, (wa pili kushoto) na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (wa kwanza kushoto) wakifuatilia mada wakati wa semina ya kuwajengea uelewa wabunge katika Sekta ya Umeme na Nishati Safi ya Kupikia, iliyofanyika Jijini Dodoma, Mei 27, 2023.*




*Mkurugenzi Mtendaji kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, akiwasilisha mada wakati wa semina ya kuwajengea uelewa wabunge katika Sekta ya Umeme na Nishati Safi ya Kupikia, iliyofanyika Jijini Dodoma, Mei 27, 2023.*



*Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy akiwasilisha mada wakati wa semina ya kuwajengea uelewa wabunge katika Sekta ya Umeme na Nishati Safi ya Kupikia, iliyofanyika Jijini Dodoma, Mei 27, 2023.*



*Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki Mhe. Miraji Mtaturuma, akizungumza jambo wakati wa semina ya kuwajengea uelewa wabunge katika Sekta ya Umeme na Nishati Safi ya Kupikia, iliyofanyika Jijini Dodoma, Mei 27, 2023.*

**JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**







## *Fika Ofisi ya Mawasiliano,*


**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**

Wasiliana nasikwa **simu namba:** +255-26-2322018

**Nukushi:** +255-26-2320148